BARAZA LA WAWAKILISHI

ZANZIBAR

TAARIFA KUHUSU MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA UCHUMI NA UWEKEZAJI YA BARAZA LA WAWAKILISHI JUU MSWADA WA SHERIA YA USALAMA NA AFYA KAZINI

MWAKA 2026

[Imetolewa kwa mujibu wa Kanuni 96(4) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Zanzibar Toleo la 2026]

Novemba, 2026

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Maelezo ya Awali

Mhe. Spika, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Allah mwingi wa Rehma kwa kuendelea kutupa neema ya uhai tunayoendelea kuitumia hadi muda huu. Aidha, tunamshukuru na kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Zanzibar Dr. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa busara na hekima zake katika kuiongoza Zanzibar. Busara na hekima hizo zinaendelea kuacha alama ya maendeleo kwa Wazanzibari wote hususan kupitia Wizara hii aliyoiunda upya kwa malengo mapana ya kutimiza ahadi za Chama Cha Mapinduzi katika kuondosha umasikini na utegemezi ndani ya jamii yetu, hakika hakuna hata mmoja wetu ambae hajaguswa na kasi ya maendeleo ya Jemedari wetu.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa Kamati yangu pia kukushukuru wewe binafsi na uongozi mzima Wa Baraza la Wawakilishi kwa jinsi mnavyotuongoza sisi wajumbe wa Baraza hili Tukufu. Busara na ushupavu wenu umeweza kuufanya Mhimili huu kuwa imara na wenye weledi katika kutimiza majukumu yake ya kikatiba.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mhe. Hemed Suleiman Abdulla,

Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa ushauri ambao amekua akitupatia mara kwa mara katika kuhakikisha kuwa tunatekeleza majukumu yetu ya kuwakilisha wananchi wetu katika kuisimamia Serikali yetu hii adhimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya awali, kabla sijawasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Baraza ya Uchumi na Uwekezaji kuhusu Mswada wa Sheria Ya Usalama na Afya Kazini, Mwaka 2026, naomba uniruhusu nimshukuru Kaka yangu, Mheshimiwa comrade Ali Suleiman Mrembo, Waziri wa Kazi, Ajira, Vijana na Uwezeshaji kwa spidi kubwa aliyoanza nayo katika kuisiamia Wizara hii, hakika tumepata jembe.

Mheshimiwa Spika, Mswada huu ulisomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Nne, na baada ya hapo ulielekeza kupelekwa katika Kamati ya Kudumu ya Baraza ya Uchumi na Uwekezaji kwa mujibu wa Kanuni ya 94(1) ya Kanuni za Baraza. Kwa kuzingatia masharti hayo, Kamati ilifanya kazi ya uchambuzi na kuandaa maoni yake.

1.2 Namna Kamati Ilivyofanya kazi

Mheshimiwa Spika, Kamati ilianza kazi ya uchambuzi kwa kutumia njia zifuatazo:-

i. Kufanya mapitio ya jumla ya maudhui ya Mswada ulioletwa kwenye

Kamati tarehe 16 Novemba, 2026;

ii. Kusikiliza na kupokea maoni ya wadau kwa mujibu wa Kanuni ya 94 (6) ya Kanuni za Baraza tarehe 17 Novemba, 2026 kwa lengo la kupata mtazamo wa umma kuhusu Mswada wa Sheria hii;

iii. Kamati iliwasilisha Jadweli la Mapendekezo ya Marekebisho kwa Waziri Kazi, Ajira, Vijana na Uwekezaji tarehe 17 Novemba, 2026 na tuliweza kukutana pamoja kwa majadiliano tarehe 18 Novemba, 2026

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuwashukuru wadau waliofika mbele ya Kamati hii na kutoa maoni yao yaliyochangia kuuboresha Mswada huu. Kipekee naomba kutambua mchango wa wataalamu mbali mbali kutoka Serikalini, Taasisi na Jumuia binafsi Zanzibar ambao kwa pamoja imeisaidia Kamati kupata taaswira pana juu ya masuala ya usalama wa afya kazini.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA MSWADA

2.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Mswada huu ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Jadweli la Kwanza chini ya Kanuni ya 123 ya Kanuni za Baraza.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanyika ulijielekeza katika masuala ya jumla kuhusiana na maudhui, masharti, mpangilio na madhumuni ya Mswada huu unaopendekezwa na Serikali. Vilevile, Kamati ilitathmini masuala mahsusi ikiwemo utekelezaji masharti (applicability) pamoja na masuala mengine katika Vifungu vya Mswada huu.

2.2 Upembuzi wa Maudhui ya Mswada

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo ya Serikali, Kamati imebaini kwamba, Mswada huu unapendekeza kufuta Sheria ya Usalama na Afya Kazini, Nam. 8 ya 2005 na kutunga Sheria mpya ya Usalama na Afya Kazini Zanzibar kwa madhumuni ya kuanzisha Mamlaka yenye uwezo na jukumu la kusimamia, kudhibiti, kuratibu na kutekeleza masuala ya usalama na afya kazini katika sehemu za kazi Zanzibar

ili kuimarisha mfumo wa usimamizi, udhibiti na ukaguzi wa usalama na afya kazini kwa kuzingatia viwango na Kanuni za Ukaguzi za Shirika la Kazi Duniani.

Mheshimiwa Spika, ili kujiridhisha na malengo ya utungwaji wa sheria hiyo inayopendekezwa, Kamati ilipitia jina refu la Mswada na sehemu ya madhumuni na sababu. Kwa kufanya hivyo, Kamati iliweza kuoanisha ahadi za Serikali kwa wananchi kuhusu usimamizi wa masuala ya usalama na afya kazini yanayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, jina refu linabainisha kuwa mapendekezo haya yanalenga kuanzishwa kwa Mamlaka yenye umadhubuti wa kisheria utakaoimarisha usimamizi na utekelezaji wa masuala ya usalama na afya kazini ili kuendana na mabadiliko mazingira ya kazi, maendeleo ya sayansi na teknolojia pamoja mabadiliko ya aina ya mifumo ya ajira. Kwa msingi huo, Kamati ilitafakari kwa upana zaidi kila kifungu ili kuona iwapo kinaboresha masharti ya utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka hiyo inayopendekezwa.

2.3 Uchambuzi Kuhusu Masharti ya Vifungu Mbalimbali vya Mswada

Mheshimiwa Spika, katika kufahamu maudhui na masharti ya Mswada huu, Kamati ilitafakari sababu na madhumuni yaliyoelezwa na mtoa hoja ili

kupata mantiki ya kila kifungu na kulinganisha na madhumuni ya jumla ya mapendekeo ya marekebisho.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha maudhui ya Mswada huu, Kamati ilitoa ushauri na mapendekezo stahili kwa kila kifungu cha Mswada huu. Napenda kulijulisha Baraza kwamba, kwa sehemu kubwa, Serikali imekua sikivu na kufanyia kazi ushauri na mapendekezo ya Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa lengo la kufanya rejea na kumbukumbu ya Baraza lako Tukufu, naomba nitoe ufafanuzi wa baadhi ya vifungu ambavyo Kamati ilitoa ushauri wake kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mswada huu unapendekeza kusimamia masuala ya afya kazini, ili kuendana sawa na mantiki hiyo, kamati imependekeza kurekebishwa kwa kufuta ufafanuzi wa neno **"afya"** katika **Kifungu cha 3** na badala yake ni kuweka ufafanuzi ufuatao:

> ***"afya"*** *maana yake ni hali ya ustawi wa kimwili, kiakili na kijamii wa mfanyakazi inayohusiana na kazi, na inajumuisha kinga dhidi ya magonjwa, madhara na hali nyingine zinazoweza kuathiri afya ya mfanyakazi kutokana na mazingira au shughuli za kazi.*

Mheshimiwa Spika, kamati inapendekeza kurekebishwa kwa ufafanuzi wa neno **"mwajiri"** kufuta maneno **"kumpa kazi mtu yeyote na kumlipa"**

yaliopo baina ya neno **“au”** na **“mtu”** na kuweka badala yake maneno **“anampa kazi mtu yeyote na anamlipa”** ili kuweka usahihi wa matumizi ya maneno, na matumizi muafaka ya istilahi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imependekeza kuongeza ufafanuzi wa neno jipya **“mtumiaji”** ambalo tunaomba likae katika mpangilio wake wa kialfabeti kama ifuatavyo:

> **“mtumiaji”** *maana yake ni mtu mwenye dhamana ya usimamizi na udhibiti wa eneo husika, hata kama sio mmiliki wa eneo hilo.*

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kurekebishwa kwa **Kifungu cha 18 aya ya (a)** kwa kufuta maneno **“fedha zilizoidhinishwa”** na kuweka badala yake maneno **“kiwango cha fedha kama kinavyoweza kuidhinishwa”.** Lengo ni kuwa na uwiano baina ya nakala za Mswada husika.

Mheshimiwa Spika, katika kuweka usahihi wa nambari katika kifungu cha 26, Kamati inapendekeza kuingiza kifungu kidogo cha **(1)** baada ya nambari 26 ambacho kimsingi kina vifungu vidogo viwili

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kurekebishwa kwa **Kifungu cha 26 (1) aya ya (k)** kwa kufuta maneno **“kinachoweza kuhatarisha”** na kuweka badala yake maneno **“kinaweza kuleta hatari kwa”** ili kuweka

urahisi wa kusomeka na kufahamika vyema.

Mheshimiwa Spika, katika kusomeka kwa urahisi na ukamilifu kwa **Kifungu cha 32,** Kamati imependekeza kurekebishwa kwa kufuta maneno yafuatayo

> *"itapitia hatua zilizochukuliwa ili kuhakikisha usalama na afya ya waajiriwa katika sehemu ya kazi husika"* na kuweka badala yake maneno;
>
> *"itapitia na itafuatilia mara kwa mara hatua zinazochukuliwa ili kuhakikisha usalama na afya ya wafanyakazi katika eneo husika la kazi".*

Mheshimiwa Spika, katika kuweka uwiano wa kimantiki baina ya nakala ya Kiingereza na Kiswahili, Kamati inapendekeza kufuta na kuandika upya kifungu cha 33 kifungu kidogo cha (2) aya ya (c) kama ifuatavyo:

> *"kuweka taratibu za kuhakikisha usalama na afya kuhusiana na utumiaji, ushughulikiaji, uhifadhi na usafirishaji wa vifaa na vitu".*

Mheshimiwa Spika, katika kuweka mtiririko mzuri wa kisheria Kamati inapendekeza kurekebishwa kwa Kifungu cha 43 kifungu kidogo cha (1) kwa kufuta maneno **"kilichoainishwa litakalopatikana kwa urahisi"** mwisho wa kifungu kidogo hicho na kuweka badala yake maneno **"kama**

ilivyoainishwa katika kanuni". Marekebisho haya yatawezesha kuainisha sehemu ambayo itaeleza kiwango kilichokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza uimara wa lugha yenye kusomeka na kufahamika kwa haraka, Kamati hii imependekeza kufuta neno "**kizuizi"** katika kifungu kidogo cha (2) na katika **Kifungu cha 47** na kuweka neno **"uzio"** ili kupatikana kwa uwiano wa maneno yaliyotumika katika Mswada.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kufutwa kwa Kifungu cha 49 kifungu kidogo cha (2) na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

> *"Kila kifaa cha mkandamizo wa hewa hakitotumika isipokuwa kifaa cha usalama kilichomo ndani yake kinafanya kazi ipasavyo."*

Lengo la marekebisho hayo ni kuweka urahisi wa kusomeka na kufahamika vyema.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo ya lugha, katika kifungu cha 50 kifungu kidogo cha (1) Kamati imependekeza kufuta aya ya **(b)** na kuandika upya kama ifuatavyo:

> *"utaratibu wa upimaji na uchunguzi utawekwa kila baada ya muda ili kuhakikisha bidhaa zake ni salama kwa matumizi yaliyokusudiwa".*

Mheshimwa Spika, katika umuhimu wa kutoa elimu juu ya matumizi ya vitu vyenye sumu, Kamati imependekeza kuongeza aya mpya ya (a) kifungu kidogo cha 6 katika Kifungu cha 56 ambacho kitasomeka kama ifuatavyo;

“kutoa elimu ya kinga na uelewa kuhusiana athari ya vitu vyenye sumu”.

Mheshimwa Spika, uboreshaji wa maeneo hayo utasaidia Baraza kutunga Sheria madhubuti itakayoboresha usimamizi wa masuala ya afya kazini ili kuweza kuwalinda wananchi wetu dhidi ya majanga yanaweza kuzuilika.

Aidha, napenda kulijulisha Baraza lako Tukufu kuwa, Serikali ilikubaliana na Kamati na kuandaa jedwali la marekebisho kwa ajili ya kujadiliwa na Barazani kwa pamoja na Mswada huu.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI YA KAMATI

3.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kuwa lengo la Kamati ni kuweza kutoa maoni mbele ya Baraza lako Tukufu juu ya Mswada huu ikiwa ni pamoja na kuliwezesha Baraza kutambua iwapo Mswada uliowalishwa unafaa, unatija au haufai kwa maslahi ya Wananchi tunaowawakilisha na visiwa vyetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na Wizara kuwa Mswada huu unalenga kuimarisha uwezo wa Serikali katika kusimamia, kudhibiti na kutekeleza masuala ya usalama na afya kazini kwa kuweka mfumo madhubuti na endelevu wa kisheria unaolenga kuzuia majanga na magonjwa yatokanayo na kazi ndani ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi uliofanyika umegusa sehemu zote za Mswada ikiwemo jina refu, vifungu vyote na sehemu ya sababu na madhumuni ya Mswada. Kwa upande wa vifungu vilivyochambuliwa, tunaipongeza sana Wizara hii kwa kupokea maoni na ushauri wa Kamati kama Jedwali la Marekebisho lilivyowasilishwa kwao.

3.2 Maoni ya Jumla

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo kuhusu matokeo ya uchambuzi, sasa naomba kutoa maoni ya jumla kama ifuatavyo: -

(i) Wizara kuhakikisha kuwa maudhui yalioainishwa kifungu kwa kifungu katika Mswada uliochapishwa kwa lugha ya Kingereza kuendana sawa na ule uliopo kwa lugha ya Kiswahili;

(ii) Serikali kuhakikisha kuwa Mamlaka inayoanzishwa ndani ya Sheria hii inasimamia ipasavyo masuala ya Usalama na Afya Kazini;

(iii) Mamlaka kutoa elimu pana kwa Wakuu wa Taasisi mbali mbali za Serikali na Waajiri binafsi juu ya masuala ya afya kazini;

(iv) Kupitia vyema Mswada huu ili kuondosha makosa ya uchapaji, maudhui na mtiririko wa maneno ili kuweka uandishi bora wenye kuleta maana inayokusudiwa; na

(v) Iwapo Mamlaka hii itawezeshwa kikamilifu italeta mafanikio chanya na mageuzi makubwa katika kulinda afya na ustawi wa wafanyakazi katika mazingira yao ya kazi

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Maelezo

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena naomba kukushukuru kwa uamuzi wako wa kutuletea Mswada huu wa Sheria ya kufuta Sheria ya Usalama na Afya Kazini, Nam. 8 ya 2005 na kutunga Sheria mpya ya Usalama na Afya Kazini ikiwa ni pamoja na kuweka Mambo mengine yanayohusiana na hayo kwenye Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, nawashukuru wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Uchumi na Uwekezaji ya Baraza la Wawakilishi kwa ushirikiano mkubwa waliokuwa nao wakati wa uchambuzi wa Mswada huu.

Mheshimiwa Spika, naamini kwa taarifa hii Baraza lako Tukufu litakuwa katika nafasi nzuri ya kuamua kwa kuzingatia maslahi mapana ya nchi yetu na wananchi wetu kwa ujumla. Kwa kutambua mchango wa Wajumbe hao, naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Baraza *(Hansard).* Majina hayo ni kama yafuatayo:-

i.	Mhe. Makame Mohammed Sufiani	Mwenyekiti
ii.	Mhe Dr. Mahmoud Omar Mohammed	M/Mwenyekiti
iii.	Mhe. Alley Masoud Alley	Mjumbe

iv.	Mhe. Shafi Mohammed Shafi	Mjumbe
v.	Mhe. Chumu Kombo Khamis	Mjumbe
vi.	Mhe. Fatma Ramadhan Mandoba	Mjumbe
vii.	Mhe. Toufiq Salim Turky	Mjumbe
viii.	Ndg. Talib Enzi Talib	Katibu
ix.	Ndg. Abdu Maulid Haji	Katibu
x.	Ndg. Shaaban Suleiman Juma	Katibu Bajeti

Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru tena Comrede Ali Suleiman Ameir (Mrembo), Waziri wa Kazi, Ajira, Vijana na Uwezeshaji ambae kwa wakati wote alikua pamoja na Kamati hii kuhakikisha kuwa tunapata kila tunachohitaji katika uchambuzi wa Mswaada huu. Aidha, shukrani zetu pia kwa Manaibu Waziri, **Mheshimiwa Seif Kombo Pandu na Mheshimiwa Zawadi Amour Nassor** wakisaidiwa na Katibu Mkuu wa Wizara hii **Mama yetu Salama Mbarouk Khatib** pamoja na Naibu Katibu Mkuu **Ndg. Khalid Masoud Wazir** Wataalamu mbalimbali kutoka Serikalini wakiongozwa na Mkurugenzi Idara ya Usalama na Afya Kazini, Dkt. **Mansour Maulid Mshenga** kwa ufafanuzi walioutoa wakati wa uchambuzi wa Mswada huu. Ufafanuzi huo na maelezo yao yamesaidia kufanikisha kazi ya uchambuzi wa Mswada huu kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, naomba nitoe pongezi

zangu za dhati kwa Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ndg. Hassan Ali Haji kwa uteuzi aliopata hivi karibuni. Hii inaonyesha ni jinsi gani Mhe. Rais wa Zanzibar amemuamini katika kuiongoza Afisi ya Baraza la Wawakilishi, tunamtakia kila kheri katika majukumu haya na tupo tayari kumsaidia kutimiza wajibu wake. Aidha, nawashukuru watumishi wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo wakati wote hadi kukamilika kwa taarifa hii.

4.2 Msimamo wa Kamati kuhusu Hoja

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Uchumi na Uwekezaji ya Baraza la Wawakilishi inalishauri Baraza lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Mswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama ilivyowasilishwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

.....

Mhe. Makame Mohammed Sufiani,
Mwenyekiti,
Kamati ya Uchumi na Uwekezaji,
Baraza La Wawakilishi,
Zanzibar.